

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA

30 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA TAREHE 30 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

479. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Mlowo Wilayani Mbozi.

480. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Itenka - Nsimbo.

481. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itagawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga na kupata Halmashauri mpya ya Kingonsera.

482. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha kuweka changarawe katika barabara inayounganisha Tarafa za Umba, Mlalo, Mtae ya Hekicho, Lugurua hadi Manolo.

WIZARA YA KILIMO:

- 483. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la uhakika la Zao la Mihogo.

WIZARA YA UCHUKUZI:

- 484. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINKIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua kipande cha Reli kinachoingia Uwanja wa Ndege KIA kwa ajili ya kusafirisha mizigo.

WIZARA YA UJENZI:

- 485. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini matengenezo ya Pantoni ya Mv Magogoni iliyopo nje ya Nchi yatakamilika na kurejeshwa nchini ili ianze kutoa huduma kwa Wananchi.

486. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itatekeleza mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kisangara - Nyumba ya Mungu kwa kiwango cha lami.

487. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango lami Barabara ya Utigi hadi Kilongwe.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UJENZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
30 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**